Jitihada nyingi zimekuwa zikifanyika duniani kote kuhakikisha wanawake wanalindwa dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia na aina zote za ubaguzi. Kutungwa kwa sheria za kimataifa kama vile Mkataba wa Afrika wa Haki za Wanawake na Watoto na Mkataba wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake ni mojawapo tu ya mifano michache ya kupambana na unyanyasaji wa kijinsia.

Hata hivyo matumizi mabaya ya madaraka yanayoambatana na unyanyasaji wa kijinsia (rushwa ya ngono) haukupewa kipaumbele mpaka hivi karibuni ambapo tumeshuhudia juhudi mbalimbali za kutokomeza unyanyasaji huu. Mojawapo ya juhudi hizo ni kuwa na neno moja la Kiingereza 'Sextortion' ambalo litasaidia kuelezea dhana nzima ya matumizi mabaya ya madaraka yanayohusisha udhalilishaji wa kijinsia au kwa lugha nyingine, rushwa ya ngono.

'SEXTORTION' NI NINI?

Huu ni msemo mpya wa kiingereza unaotumika kuelezea dhana ya matumizi mabaya ya madaraka yanaoambatana na unyanyasaji wa kijinsia (rushwa ya ngono). Wanawake na wanaume huathirika na 'sextortion' japokuwa waathirika wakuu ni wanawake.

MAZINGIRA YA 'SEXTORTION'

- Kuonyesha sehemu za siri za mwili kwa mwanafunzi, muumini, mgonjwa, mtu aliye kizuizini
- Kupiga picha za uchi.
- Kugusana, kufinyana, kusuguana na kupapasa sehemu za siri
- Kubaka na kunajisi.

N.B kwa ujumla tunapozungumzia "sextortion" hatuzungumzii tendo au tabia ambazo hazihusiani na ngono.

RUSHWA KAMA MOJAWAPO YA KIGEZO CHA 'SEXTORTION'

1. Mhusika wa kitendo cha kudai rushwa ya ngono lazima awe na madaraka au mamlaka ambayo anayatumia vibaya kudai rushwa ya ngono au kukubali rushwa ya ngono katika kutumia madaraka hayo ili kumtekelezea mlengwa hitaji lake.
2. Rushwa ya ngono hutumika kukidhi haja ya mwenye madaraka badala ya kuzingatia sifa za mhanga, sheria, au maadili husika.



Kwa kifupi ngono ndiyo inayotumika katika rushwa na siyo fedha

Tendo la rushwa lina vigezo vitatu

1. **Kutumia madaraka vibaya**
   - ❖ Madaraka yanaweza kuwa ya:
   - ❖ Kisheria
   - ❖ Kidini
   - ❖ Kikazi

Kitu cha msingi cha kuzingatia ni kwamba hayo mamlaka ni lazima yawe halali kisheria.

2. **Aina ya rushwa inayotumika katika ubadilishaji ni hiki kwa kile**

Madaraka yanatumiwa kumnyanyasa mlengwa kijinsia ili aweze kupata hitaji lake.

3. **Unyanyasaji unaoumiza ndani kwa ndani ambao si lazima kutumia nguvu.**

NI MADHARA GANI JAMII INAPATA KUTOKANA NA 'SEXTORTION'?

Matumizi mabaya ya madaraka yanayohusisha unyanyasaji wa kijinsia (Sextortion) yana athari kubwa katika jamii yetu kama ifuatavyo:

- Yanaongeza maambukizi ya ukimwi,
- Yanadhalilisha utu
- Yanashusha utendaji na kurudisha maendeleo nyuma
- Yanasababisha migogoro katika familia na hasa mafarakano katika ndoa na ongezeko la watoto wa mitaani na malezi duni

'SEXTORTION' KATIKA TAASISI ZA KIDINI

Neno 'sextortion' laweza kutumika kuelezea matendo ya udhalilishaji kijinsia, na ngono ya rushwa yanayofanywa na viongozi wa kidini dhidi ya waumini.

MIFANO YA 'SEXTORTION' KATIKA TAASISI ZA KIDINI

Kiongozi wa kidini anaweza kumdhalilisha kijinsia muumini kwa kumshika sehemu zake za siri wakati akimfanyia maombi au akimpa ushauri au huduma nyingine.

Kiongozi wa kidini anaweza kuomba rushwa ya ngono kutoka kwa muumini ili amuombee au amuombee ndugu au rafiki yake.

Kiongozi wa kidini anaweza kuomba rushwa kutoka kwa mfanyakazi wa kanisani ili achaguliwe kwenye kamati.

RUSHWA YA NGONO KWENYE TAASISI YA KIDINI IMEGAWANYIKA KATIKA VIGEZO VIWILI

Kutumia madaraka vibaya

Kutokana na imani iliyojengeka kwa waumini kuwa kiongozi wa kidini ana nguvu za kiroho hivyo inakuwa vigumu kwa waumini kupinga au kukataa ombi la rushwa ya ngono kutoka kwa kiongozi huyo.

Hiki kwa kile (quid pro qui)

Kama kiongozi wa kidini madaraka aliyonayo dhidi ya watumishi wa chini ni makubwa, kwa mfano kupendekeza watumishi kupandishwa vyeo au kuwa pandishwa vyeo yeye binafsi. Bila shaka itamuwia vigumu mtumishi yeyote kupinga ombi la rushwa ya ngono ili apandishwe cheo.

'SEXTORTION' KATIKA FANI YA UTABIBU

Katika nyanja ya utabibu, sextortion inamhusisha daktari dhidi ya wagonjwa, rafiki au ndugu wa wagonjwa. Katika hili, daktari hutumia vibaya dhamana aliyonayo juu ya mgonjwa kwa kukiuka maadili ya kazi yake pale anapodai rushwa ya ngono ili aweze kumtibu mgonjwa huyo. Daktari anapolazimisha kwa nguvu kitendo cha ngono dhidi ya mgonjwa ni ubakaji. Lakini pale anapotumia madaraka yake kudai rushwa ya ngono ili mgonjwa apate matibabu, hii ni sextortion.

MIFANO YA 'SEXTORTION' KATIKA FANI YA UTABIBU

Daktari anaweza kumpapasa au kumshika sehemu za siri mgonjwa kwa minajili ya kujifurahisha kimapenzi wakati akimfanyia uchunguzi wa kitabibu.

Mgonjwa asiyeweza kugharamia matibabu yake anaweza kuombwa rushwa ya ngono na daktari ili apatiwe matibabu bure.

Daktari anaweza kutumia nguvu kumdhalilisha kijinsia mgonjwa.

RUSHWA YA NGONO KWENYE FANI YA UTABIBU IMEGWANYIKA KATIKA VIGEZO VIWILI

Kutumia madaraka vibaya

Daktari anaweza kumdhalilisha kijinsia mgonjwa wakati akimfanyia utafiti wa kitabibu. Kutokana na kutokuwa na uelewa wa masuala ya kitabiu mgonjwa anaweza asitambue kwamba kitendo anachokifanya daktari sio sahihi.

Hiki kwa kile (quid pro qui)

Daktari anaweza kukataa kutoa huduma ya matibabu ambayo inatolewa bure mpaka atakapopewa rushwa ya ngono ndipo aweze kumhudumia mgonjwa.

'SEXTORTION' KATIKA MAZINGIRA YA KAZI

Matumizi mabaya ya madaraka yanayohusisha rushwa ya ngono yanaweza kujitokeza sehemu zote za kazi mfano katika ajira za majumbani, utumishi wa umma, mahakamani nk. Mara nyingi, watu huogopa kukataa jambo lenye mahusiano ya kingono na viongozi wenye madaraka juu yao kwa kuhofia kupoteza ajira

au nafasi nzuri kazini au stahili zao. Wengi hujikuta wamejiingiza katika mahusiano ya kingono bila kupenda.

MIFANO YA 'SEXTORTION' KATIKA MAENEO YA KAZI

Mtu aliye na madaraka katika sehemu za kazi anaweza kumtaka mtu wa chini yake afanye naye ngono ili apate upendeleo katika kupandishwa cheo, malipo, na nafasi nzuri kazini.

Au mtu anayestahili kupandishwa cheo au kupewa malipo fulani hapatiwi kama anavyostahili bila kutimiza sharti la kufanya ngono na mtu aliye na madaraka ambaye ndiye mwenye jukumu la kutoa stahili husika.

'SEXTORTION' KATIKA POLISI NA MAGEREZA

Hii inaweza hutokea katika mifano ifuatayo;

- Afisa magereza au polisi kumtaka kingono mfungwa au mtu aliye mahabusu ili apate upendeleo fulani akiwa kizuizini.
- Afisa magereza kutaka mahusiano ya kingono kama sharti la kuruhusu ndugu kutoa huduma fulani kwa mwenzao aliyepo kizuizini
- Afisa wa polisi au magereza kumbaka mtu aliye kizuizini ndani ya gereza au selo ya polisi

'SEXTORTION' MASHULENI NA VYUONI

Mashuleni na vyuoni watoto wa kike na wa kiume hurubuniwa kwa vitu kama kuahidiwa kusaidiwa katika mitihani, kupewa alama za juu ili watoe miili yao kwa wakuu wao.

Madhara ya 'sextortion' mashuleni

- Utoro pale ambapo mototo wa kike au kiume atajisikia kudhalilika akigundulika kuwa ana mahusiano ya kingono na mwalimu wake.
- Mimba za utotoni
- Magonjwa ya zinaa
- Kushuka kwa viwango vya elimu

Je, kosa la 'sextortion' linaweza kushughulikiwa katika sheria gani?

- Linaweza kushughulikwa chini ya sheria mbalimbali:
  -Kanuni za adhabu kifungu cha 130(3) kinachukulia matumizi mabaya ya madaraka yanayohusisha udhalilishaji wa kijinsia kama kosa la kubaka.
  -Sheria ya kuzuia na Kupambana na Rushwa 2007 kifungu cha 25 kinatambua 'sextortion' kama kosa la rushwa

KWA NINI NI MUHIMU KUSHUGHULIKIA 'SEXTORTION'?

- Viko vitendo vingi vya 'sextortion vinavyofanyika katika ofisi mbalimbali- mashuleni, hospitalini, waganga wa jadi, viongozi wa dini, magereza, polisi nk. lakini havitolewi taarifa.
- Tunataka jamii itambue athari za vitendo hivi ikiwa ni pamoja na maambukizi ya ukimwi, kushuka kwa utendaji, nidhamu mahali pa kazi nk.
- Tunataka wahanga watiwe moyo kutoa taarifa ya vitendo hivi ili viweze kuchukuliwa hatua na hatimaye vikemewe na kutokomezwa

MUATHIRIKA WA 'SEXTORTION' ANAWEZA KUFANYA NINI?

KATIKA TASISI ZA KIDINI

Anaweza kutoa taarifa kwenye kamati inayohusika na maadili ya viongozi wa dini husika.

Anaweza kutoa taarifa polisi au kwenye taasisi inayoshughulikia rushwa nchini Tanzania.

POLISI

Akitoa taarifa polisi mshatakiwa anaweza akashitakiwa chini ya kifungu namba 130 cha Kanuni za Adhabu kama kosa la ubakaji au udhalilishaji wa kijinsia.

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Akitoa taarifa kwenye taasisi iliyotajwa hapo juu mshitakiwa anaweza akashitakiwa chini ya kifungu namba 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, 2007 ambayo imefanya 'sextortion' kuwa mojawapo ya viendo vya rushwa

KATIKA FANI YA UTABIBU

Muathirika anaweza kutoa taarifa kwenye chama cha madaktari Tanzania (MAT) Malengo ya chama hiki ni kusimamia maadili ya kitabibu na matendo ya madaktari Tanzania.

Anaweza pia kutoa taarifa polisi au kwenye Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa hatua zaidi za Kisheria.

Katika Tasisi za Elimu, Magereza na hata Polisi, kunapotokea dalili za matumizi mabaya ya madaraka yanayoambatana na udhalilishaji wa kijinsia muathirika anaweza kutoa taarifa kwa kiongozi wa mhusika na udhalilishaji ule na pia anaweza kutoa taarifa polisi au Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa hatua za kisheria.

Inawezekana kuitokomeza 'sextortion' kwa:

- kutoa taarifa
- kuzingatia uadilifu
- kutii sheria.
- Kutoa elimu ya haki za binadamu na 'sextortion' mashuleni na kwa jamii kwa ujumla

TAWJA

International Association of Women Judges

UNAWEZA KUZUIA NA KUPAMBANA NA MATUMIZI MABAYA YA MADARAKA YANAYOAMBATANA NA UDHALILISHAJI NA UNYANYASAJI WA KIJINSIA (SEXTORTION) MASHULENI, VYUONI, MAHALI PA KAZI, MAHOSPITALINI, MAJUMBANI NA KATIKA TAASISI ZA DINI

PROGRAMU YA KUTOKOMEZA MATUMIZI MABAYA YA MADARAKA YANAYOAMBATANA NA UNYANYASAJI WA JINSIA; KUTAMBUA, KULAANI NA KUTOKOMEZA SEXTORTION

PROGRAMU HII IMEFADHILIWA NA WIZARA YA MAMBO YA NJE YA SEREKALI YA UHOLANZI KUPITIA MFUKO WA MDG3 KWA AJILI YA TANZANIA, BOSNIA-HERZEGOVINA NA UFILIPINO(2009-2011)

Development Cooperation
Ministry of Foreign Affairs